# UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 13 Machi, 2023



# MKURUGENZI WA UCHAGUZI AKABIDHIWA OFISI

IFAHAMU TUME

# UBORESHAJI WA DAFTARI

**Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi,
Sura ya 343 na Kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali
za Mitaa, Sura ya 292, Tume inatakiwa kuboresha Daftari la Kudumu
la Wapiga Kura mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu uliomalizika na
unaofuata. Wanaohusika katika zoezi hili ni wananchi ambao: -

(i) Wametimiza umri wa miaka 18 na kuendelea ambao
hawakuandikishwa hapo awali;

(ii) Watakaotimiza miaka 18 wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2020;

(iii) Waliojiandikisha awali na wamehama Kata au Jimbo moja
kwenda jingine;

(iv) Waliokosa sifa mfano wale waliofariki kuondolewa katika
Daftari;

(v) Wenye taarifa zilizokosewa wakati wa uandikishaji; na

(vi) Waliopoteza au kadi zao kuharibika.



# Mkurugenzi wa Uchaguzi akabidhiwa Ofisi

**_Na Mwandishi wetu_**

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Ramadhani Kailima. amekabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa tume hiyo Dkt. Mahera Wilson Charles ambaye sasa ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya.

Hafla hiyo ya makabidhiano imefanyika Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yaliyopo Njedengwa jijini Dodoma tarehe14 Machi, 2023.

Makabidhiano hayo yamefanyika kufuatia, Rais Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko ya Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi tarehe 26 Februari,2023 kwa kumteua Bw. Kailima kushika wadhifa huo, huku Dkt. Mahera akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya.




Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Bw. Ramadhani Kailima alimshukuru mtangulizi wake kwa maandalizi aliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa shughuli zote za Tume zipo kwenye ratiba jambo ambalo litarahisisha utendaji kazi wa ofisi hiyo.

"Ninashukuru sana na ninakupongeza Dkt. Mahera kwani nimekuta mambo yote yapo katika mpangilio mzuri, hii itasaidia sana kufanya kazi," amesema Bw. Kailima.

Viongozi hao waliapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kushika nyadhifa zao kwa nyakati tofauti ambapo Bw. Kailima aliapishwa Februari 27 mwaka huu, huku Dkt. Mahera akiapishwa Machi 11, 2023 katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

# Majukumu ya Tume hayaishii kwenye Uchaguzi



*Na Mwandishi wetu*

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Ramadhani Kailima amekutana na watumishi wa Tume hivi karibuni ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu ateuliwe kushika wadhifa huo.

Kwenye kikao hicho kilichofanyika kweye Ofisi za Tume jijini Dodoma, Kailima amewataka watumishi wa Tume kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia kalenda ya Uchaguzi kwa kuwa majukumu ya Tume ni mengi na hayaishii kwenye Uchaguzi Mkuu.

“Wapo watu hawajui majukumu ya Tume na utendaji kazi wake na wanahoji baada ya Uchaguzi Mkuu Tume ina kazi gani?” amesema Kailima.

Tume hufuata mzunguko wa uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu ambazo ni Kabla ya Uchaguzi Mkuu, wakati wa Uchaguzi Mkuu na baada ya Uchaguzi Mkuu.

Baadhi ya majukumu yanayotekelezwa kabla ya Uchaguzi Mkuu ni pamoja na kuandaa bajeti, ratiba ya utekelezaji, ununuzi wa vifaa vya uchaguzi, elimu ya mpiga kura, uandikishaji wa wapiga kura na kuweka wazi daftari la awali.

Aidha, majukumu yanayotekelezwa wakati wa Uchaguzi ni pamoja na Uteuzi wa wagombea, Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura, Uratibu wa Kampeni, Utekelezaji wa Maadili, Usajili wa watazamaji wa uchaguzi, Uchapishaji na usambazaji wa Karatasi za Kura, Upigaji Kura, Kuhesabu Kura na Kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

Vile vile, baadhi ya majukumu yanayotekelezwa baada ya Uchaguzi ni pamoja na Ukaguzi wa vifaa vya uchaguzi kwenye Halmashauri, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Maboresho ya Sheria, Tathmini ya mwenendo wa Uchaguzi na Taarifa ya Uchaguzi.

Bw. Kailima amesisitiza kwamba majukumu hayo ya Tume katika nyakati tofauti za mzunguko wa uchaguzi ni muhimu yatekelezwe kwa ufanisi na kuwataka watumishi wawajibike kikamilifu kwenye idara na vitengo vyao.

Mkurugenzi huyo wa Uchaguzi ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 26/02/2023 na kuapishwa tarehe 27/03/2023 Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma.





# Tume ya Taifa ya Uchaguzi yashiriki kikao cha ECF SADC nchini Angola

***Na Mwandishi wetu***

Kikao cha Watendaji Wakuu wa Jukwaa la Tume za Uchaguzi kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (ECF-SADC) kilifanyika katika jiji la Luanda nchini Angola kuanzia tarehe 13 hadi 17 machi, 2023.

Kikao hicho ambacho kiliwashirikisha Watendaji Wakuu wa Tume za Uchaguzi kutoka nchi 13 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kilihudhuriwa na Mkurugenzi wa Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Nassoro Shemzigwa ambaye alimwakilisha Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw.Ramadhani Kailima.

Kwa mujibu wa Bw.Shemzigwa, watendaji wakuu wa Tume za Uchaguzi kutoka nchi wanachama wa ECF-SADC kutoka nchi za Lesotho na Mauritius ndiyo ambao hawakuweza kushiriki kikao hicho.

Bw. Shemzigwa ameongeza kuwa kikao hicho pamoja na kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zinazohusu jumuiya ya ECF SADC ikiwemo taarifa ya maandalizi ya maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya hiyo, pia watendaji hao wakuu walipata fursa ya kupitia kijitabu cha Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Utazamaji wa Uchaguzi katika Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Mbali na kushiriki mikutano na vikao mbalimbali na shughuli za Jukwaa hilo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inanufaika na fursa nyingine zinazotolewa na jukwaa hilo zikiwemo mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi katika masuala ya uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi.

Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (ECF-SADC) ni taasisi huru ambayo inajumuisha tume za uchaguzi 15 kutoka nchi 14 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Mbali na Tanzania ambayo inawakilishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, tume za uchaguzi nyingine ni kutoka nchi za Angola, Malawi, Ushelisheli, Zambia, Zimbabwe, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Eswatini, Lesotho na Mauritius.




# Wanawake NEC Watoa Msaada Gereza Kuu Isanga

***Na Mwandishi wetu***

Watumishi wanawake wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wametoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wafungwa na mahabusu waliopo katika Gereza kuu la Isanga lililopo Jijini Dodoma.

Msaada huo ulikabidhiwa Alhamis Machi 2,2023 ikiwa ni maandalizi ya

kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo ilifanyika machi 8, 2023.

Mwenyekiti wa wanawake Tawi la TUGHE kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bi.Nuwia Sultan amesema kuwa wamefanya matendo hayo ya huruma kama Ishara ya Upendo na kuwakumbuka wanawake na watoto waliopo Magerezani.

“Matendo haya hatujafanya sisi tu tuliofika hapa, lakini pia kuna wenzetu ambao tumewaacha ofisini wakiwemo akina baba nao wameshiriki, tumeleta vitu kwa ajili ya watoto na wakina mama, kwa hiyo tunaomba vifaa hivi viwafikie walengwa kwa sababu hiki ni kipindi kitakatifu kwa pande zote mbili,” amesema Bi.Nuwia.

Vifaa hivyo ambavyo vina thamani ya shilingi 880,000 ni pamoja na taulo za kike, nepi kwa ajili ya watoto, mafuta ya kupaka, sabuni, miswaki na dawa za meno na katoni za maji.

Mbali na kukabidhi vifaa hivyo, wanawake hao kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi walichangishana na kufanikiwa kuwalipia faini ya shilingi 515,000 wafungwa wawili wanawake waliokuwa wakitumikia adhabu zao za vifungo katika Gereza hilo baada ya kuwatembelea na kubaini changamoto zilizokuwa zikiwakabili ikiwa ni pamoja na mfungwa mmojawapo kuishi na mtoto mdogo gerezani hapo.

Akizungumza mara baada ya kupokea vifaa hivyo Kaimu Msimamizi wa Idara ya Wanawake katika gereza hilo Mrakibu Msaidizi wa Magereza Yusta Ligazio amewashukuru wanawake hao kwa jinsi walivyoguswa na changamoto zinazowakabili wafungwa na mahabusu wa gereza kuu vla Isanga hususani wanawake na watoto wachanga ambao wamelazimika kuishi huko na wazazi wao.





# Kamba NEC yaibuka kidedea tamasha la michezo la Ukaguzi

***Na Mwandishi wetu***

Tamasha la Michezo lililoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kushirikisha timu kutoka taasisi 6 za Serikali zilizopo jijini Dodoma limefana kwa kufanyika kwa michezo mbalimbali ukiwemo mchezo wa kuvuta kamba ambapo timu kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliibuka kidedea na kushinda kikombe katika mchezo huo.

Katika Tamasha hilo la kusisimua, Timu ya kamba ya NEC wanaume ilipata ushindi huo baada ya kuwavuta kwa mivuto miwili Timu ya kamba ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, huku pia ikimshuhudia mchezaji Josephine Mchalange kutoka Timu ya kukimbiza kuku wanawake ya NEC akifanikiwa kumdaka Jogoo waliyekuwa wakimfukuza.

Katika Mpira wa Miguu NEC hawakufurukuta mbele ya Makao Makuu Jogging ya Dodoma baada ya kuwatupa nje kwa mikwaju ya penati ambapo katika mchezo wa fainali timu ya Makao Makuu ilikutana na Ukaguzi na Makao Makuu kushinda mchezo katika tamasha hilo.

Katika mchezo wa Mpira wa Netiboli timu ya Ukaguzi iliibuka kidedea baada ya kuzitandika bila huruma timu za Wizara ya Afya na Madini.

Mapema akizungumza wakati wa ufunguzi wa bonanza hilo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bw. Charles Kichere amewataka watumishi wa umma wakiwemo wa Ofisi yake kujenga mazoea ya kushiriki kwenye michezo kwani ni tiba isiyo na gharama hasa kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Amesema kwa kufanya hivyo wanaipunguzia Serikali mzigo wa kuhudumia wagonjwa na ndiyo maana katika kulinda afya za watumishi ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na kutumia muda mwingi kuandika taarifa wakiwa ofisini wameweka utaratibu wa kutoka nje na kufanya mazoezi mara baada ya kazi.

Mbali na watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) taasisi nyingine zilizoshiriki Bonanza hilo ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Wakala wa Barabara (Tanroads), Ofisi ya Rais Ikulu na Wizara ya Afya.



# SHAIRI

## Hongera Tume

***Na Mwandishi wetu***

Tume yetu ya taifa, ya uchaguzi nchini,
Imejipatia sifa, wengi wanaithamini,
Hutuma nyingi arafa, kusifia umakini,
Hongera kwa watendaji, chaguzi kusimamia,

Ona yake majukumu, tume inavyoyatenda,
Hata yale ya awamu, huyafanya bila inda,
Sheria huziheshimu, katika kazi kutenda,
Hongera kwa watendaji, chaguzi kusimamia,

Tangu kwake kuanzishwa, mwezi ule januari,
Mwaka tisini na tatu, malengo hayakufichwa,
Wala kufanya kiburi, wadau kukarahishwa,
Hongera tume hongera, kwa kazi zenu nzuri,

Wengi walishirikishwa, chaguzi zilizopita,
Washindi waliapishwa, bila hata ya kusita,
Haikutumika rushwa, ya pesa wala kashata,
Hongera tume hongera, amani kuidumisha,

Inasimamia haki, kuendesha uchaguzi,
Haizui taharuki, wala kufanya ajizi,
Kwa yoyote mshiriki, kila jambo kwa uwazi,
Hongera tume hongera, kwa umakini wa kazi,

Kwenye yake majukumu, yote yaliyo muhimu,
Huyafanya kwa nidhamu, bila haki kudhulumu,
Vikao vyote muhimu, vinafanyika kwa zamu,
Hongera tume hongera, kuyalinda maadili,

Vyama huvishirikisha, hima kwa kila hatua,
Mikutano huitisha, migogoro kutatua,
Kasoro kuziondosha, zile walizo ibua,
Hongera tume hongera, kwa kazi zenu nzuri,

Tume imeleta haki, usawa kwa kila chama,
Imejenga urafiki, kuondoa uhasama,
Vyama vyote hushiriki, kwa amani na salama.
Hongera tume hongera, kwa kazi zenu nzuri,

Ikifikia wakati, wa uchaguzi nchini,
Huipanga mikakati, kwa weledi na makini,
Huunda pia kamati, kwa kutumia kanuni,
Hongera tume hongera, kwa kudumisha amani,

Na makundi maalumu, nyuma hayakubakia,
Yamepewa umuhimu, popote kuyafikia,
Hata ikiwa kwa zamu, ujumbe kuwatumia,
Hongera tume hongera, wadau kushirikisha,

Jamii za wafugaji, na wavuvi madagoni,
Kando ya mto rufiji, wote wawemo kundini,
Hata wale wa ujiji, wafike mikutanoni,
Hongera tume hongera, wadau kuwafikia,

Kwa hapa nilipofika, naweka chini kalamu,
Wakati ukishafika, tupeane majukumu,
Tuyatende kwa shirika, maadili kuheshimu,
Hongera tume hongera, kwa kazi zenu nzuri.




Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania
Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV